**_Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi._**

Afya au ___1___ ni hali ya kutokuwa na magonjwa ___2___ mwilini. Mtu ___3___ mwili wake hauna ugonjwa huwa na nguvu ___4___ kufanya kazi. Mwanafunzi ___5___ afya anaweza ___6___ bila tatizo. Ili uwe na afya nzuri, unashauriwa ___7___ vyakula vinavyofaa. Pia ni vyema ___8___ usafi wa mwili na mazingira yako. ___9___ michezo kama vile kandanda, jugwe na mwajificho ni muhimu.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. zaraa | B. siha | C. aila | D. majonzi |
| **2.** | A. yoyote | B. yeyote | C. wowote | D. lolote |
| **3.** | A. ambao | B. ambaye | C. ambayo | D. ambazo |
| **4.** | A. cha | B. la | C. za | D. wa |
| **5.** | A. mwenyewe | B. mwenye | C. ambaye | D. aliye |
| **6.** | A. kusomesha | B. kusomwa | C. kusoma | D. kusomea |
| **7.** | A. kukula | B. kunywa | C. kukunywa | D. kula |
| **8.** | A. kudumisha | B. kutumbuiza | C. kudunisha | D. kutumbukiza |
| **9.** | A. Nayo | B. Nao | C. Nazo | D. Nalo |

Watu waliingia ___10___ na kuketi huku wakimsubiri ___11___ aingie na kuamua kesi. Mama ___12___ alionekana mwenye huzuni ___13___ kwenye uso wake. Kaka alikuwa ameshtakiwa ___14___ kosa la wizi. Baadaye alihukumiwa kifungo ___15___ miaka mitano gerezani.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. kotini | B. polisi | C. kwa mahakama | D. kortini |
| **11.** | A. mshtakiwa | B. polisi | C. mfungwa | D. hakimu |
| **12.** | A. yangu | B. zangu | C. wa | D. wangu |
| **13.** | A. mingi | B. nyingine | C. mwingi | D. nyingi |
| **14.** | A. na | B. kwenye | C. kwa | D. katika |
| **15.** | A. ya | B. cha | C. la | D. wa |

***<u>Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.</u>***

16. Chagua ukanusho wa;
**Ninapenda kusoma.**
A. Haupendi kusoma.
B. Ninapenda kutosoma.
C. Nilipenda kutosoma.
D. Sipendi kusoma.

17. Taua sentensi yenye '**ki**' cha masharti.
A. Kijibwa kimelala chini.
B. Ukitembea haraka utaanguka.
C. Mzee huyu anatembea kijeshi.
D. Kitabu chake kimepotea.

18. Jibu lipi lenye vihusishi pekee?
A. mwenyewe, zote, vingine.
B. safi,hodari, mzuri.
C. kabla ya, baada ya, chini ya.
D. wangu, chake, lake.

19. Jaza nafasi kwa kiunganishi kinachofaa.
**Sitaki kula _______ kunywa chai.**
A. kwa sababu B. wala
C. lakini D. na

20. Chagua sentensi ambayo ni sahihi?
A. Sahani yenye uchafu imeoshwa.
B. Mikunga mingi imepikwa.
C. Mtoto mwenyewe kucheza anapendeza.
D. Kalamu yeyote itatumika na mwalimu.

21. Ni orodha ipi yenye nomino za ngeli ya **I - ZI** pekee?
A. nyumba, nyuzi, dawa.
B. chupa, karatasi, kalamu.
C. saa, kabati, karai.
D. nyuta, nywele, nyasi.

22. Ni sentensi gani iliyotumia '**karibu**' kuonyesha **nusura**?
A. Tumesimama karibu na gari.
B. Mkutano karibu uanze.
C. Nyumba karibu ianguke.
D. Karibu nyumbani mgeni wetu.

23. Neno **mkate** lina silabi ngapi?
A. 2 B. 5
C. 4 D. 3

24. Chagua sentensi iliyoakifishwa kwa kutumia alama za dukuduku.
A. Lo! Vijana wale wamefukuzwa na mbwa!
B. Ukiona vyaelea jua ...
C. "Wewe ni nani?" Mwalimu aliuliza.
D. Alinunua maembe, ndizi, tufaha na machungwa.

25. Musabye ni mwana wa Ndegwa. Janice ni mke wa Musabye. Ndegwa atamwitaje Janice?
A. Wifi B. Babamkwe
C. Mkazamwana D. Mkazamjomba

26. Shairi lenye mishororo minne katika kila ubeti huitwaje?
A. Takhmisa B. Tarbia
C. Tathlitha D. Tathnia

27. Chagua wingi wa: **Mkebe wa mama umepotea ukiwa uwanjani.**
A. Mikebe za akina mama zimepotea zikiwa nyanjani.
B. Mikebe ya wamama imepotea ikiwa uwanjani.
C. Mikebe ya akina mama yamepotea yakiwa nyanjani.
D. Mikebe ya akina mama imepotea ikiwa nyanjani.

28. Ikiwa leo ni Alhamisi, juzi ilikuwa;
A. Jumanne B. Jumatatu
C. Ijumaa D. Jumamosi

29. Tambua kinyume cha;
**Shaibu ameuza jogoo mkubwa.**
A. Nyanya amenunua kuku mdogo.
B. Ajuza amenunua koo mdogo.
C. Shaibu hajauza jogoo mkubwa.
D. Ajuza amenunua kuku mdogo.

30. Chagua maamkuzi ya wakati wa jioni pekee.
A. Chewa
B. Salaam aleikum
C. Sabalheri
D. Masalheri

**_Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 hadi 40._**

Matatizo alizaliwa katika familia ya wazazi waliokuwa maskini hohehahe. Wazazi hao walikuwa hawana mbele wala nyuma. Baba yake alifanya biashara ya kuuza samaki ufuoni pa Bahari Lusumu. Mama yake aliwafulia watu nguo kwa ujira mdogo. Ingawa waliishi maisha magumu na yenye matezo tele, **hawakufa moyo**. Walijikaza kisabuni na kufanya kazi zao kwa bidii kama mchwa. Walijua kuwa **bidii huleta faida**. Baba wa Matatizo, mzee Jikaze, aliendelea na biashara yake hadi alipofungua kibanda kidogo cha samaki pale mjini Mumias. Sasa Mzee Jikaze aliendeleza biashara yake ufuoni pa bahari huku mkewe naye akiuza kibandani pale mjini Mumias.

Matatizo alisomea katika shule ya umma karibu na mji wa Mumias. Kwa sababu ya uchache wa pesa, Matatizo hakuwa na viatu wala vitabu vyote vilivyohitajika. Kila asubuhi na jioni, alivumilia uchungu wa kudungwa na mawe pale barabarani alipoenda au kutoka shuleni. Alifahamu kuwa mvumilivu hula mbivu. Wanafunzi wenzake walipochezacheza darasani, yeye aliwaomba wenzake vitabu na kujisomea kwa uangalifu. Hakupoteza muda akiyafanya mambo yasiyofaa.

Matatizo pia alikuwa mwenye heshima na nidhamu kwa kila mtu. Aliwaheshimu wakubwa kwa wadogo. Wazazi na walimu walimtumia kuwa mfano kwa watoto na wanafunzi wao. Kila mara alijizolea tuzo na zawadi za mwanafunzi bora katika usafi na nidhamu. Masomoni hakuachwa nyuma, daima alikuwa miongoni mwa wanafunzi watano wa kwanza katika mtihani. Alipomaliza masomo ya shule ya msingi, alifadhiliwa na benki moja ambayo iliwadhamini wanafunzi werevu kutoka katika familia maskini. Matatizo aliendelea kusoma na kuwaheshimu wenzake. Aidha, alianza kuibuka kuwa mwanasoka maarufu sana.

Darasani alikizika kichwa chake vitabuni kama mwanasheria atafutaye neno la ushindi katika kesi. Wakati wa alasiri, Matatizo alikuwa uwanjani na wanasoka wenzake. Walicheza kwa kushirikiana kama kiko na digali. Walielewa kuwa umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. Licha ya kufaulu katika mtihani wa kidato cha nne, Matatizo pia aliteuliwa katika timu ya taifa ya wachezaji wasiozidi umri wa miaka ishirini. Katika chuo kikuu alisomea udaktari huku akiendeleza talanta yake ya kusakata kabumbu.

Ama kwa hakika, Mola hamwachi mja wake. Mtoto wa watu aliajiriwa kuwa daktari katika hospitali kuu ya mji wa Mumias. Kila alipopata nafasi, alienda uwanjani kufanya mazoezi na kusakata kandanda na wenzake. Matatizo hakuwasahau wazazi wake, alihakikisha kuwa wameishi maisha ya raha na starehe. Pia alifungua hospitali ya kuwasaidia wanawake wajawazito kujifungua na kuyatibu magonjwa ya watoto wachanga. Hayakuishia hapo. Matatizo ndiye aliyefungua kituo cha kwanza nchini cha kukuza talanta za vijana. Maisha ya Matatizo hutumika kuwatia moyo watu wengi wanaopitia matatizo.

31. Kulingana na aya ya kwanza, ni kweli kuwa:
A. baba wa Matatizo alivua samaki ufuoni pa bahari
B. familia ya Mzee Jikaze iliteseka kutokana na umaskini
C. Mzee Jikaze alikuwa na watoto wengi
D. mama wa Matatizo hakufanya kazi yoyote.

32. Chagua jibu ambalo **si** kweli kulingana na ufahamu.
A. Mzee Jikaze alifungua kibanda kidogo cha samaki karibu na Bahari Lusumu.
B. Matatizo hakusomea katika shule ya kibinafsi.
C. Matatizo hakuchezacheza darasani kama wenzake.
D. Matatizo alikuwa mfano bora shuleni.

33. Maneno '**hawakufa moyo**' yana maana gani?
A. Hawakuaga dunia.
B. Hawakupoteza matumaini.
C. Hawakuwa wazembe.
D. Hawakuacha kufanya kazi.

34. Makala haya yanaonyesha kuwa Matatizo alikuwa mwenye tabia zipi?
A. Mwenye bidii na mchoyo.
B. Mvumilivu na mwoga.
C. Mvumilivu na mwenye bidii.
D. Mzembe na mchoyo.

35. '**... bidii huleta faida...**' Ni methali gani ambayo **haiafiki** maneno haya?
A. Mchumia juani hulia kivulini.
B. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.
C. Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.
D. Mola hamwachi mja wake.

36. Kulingana na **aya ya tatu**, ni kweli kuwa:
A. Matatizo alikuwa akiwaongoza wenzake masomoni kila wakati
B. Matatizo alikuwa mwanafunzi safi na mwenye nidhamu
C. Matatizo alikuwa nambari ya tano katika kila mtihani
D. Matatizo alifadhiliwa alipokuwa akiendelea na masomo ya shule ya msingi.

37. Uwezo wa Matatizo wa kucheza soka ulianza kujulikana akiwa katika kiwango gani cha masomo?
A. Shule ya upili.
B. Shule ya msingi.
C. Chuo kikuu.
D. Shule ya chekechea.

38. Katika chuo kikuu, Matatizo alisomea nini?
A. Kuwatibu wagonjwa.
B. Kujenga hospitali.
C. Kuwahudumia wagonjwa.
D. Kuwaombea wagonjwa.

39. Timu ya taifa ambayo Matatizo aliteuliwa kuichezea ilikuwa ya:
A. wachezaji walemavu
B. wachezaji waliozidi miaka ishirini
C. wachezaji kutoka familia maskini
D. wachezaji wa miaka ishirini kurudi chini.

40. Ni kweli kuwa wazazi wa Matatizo;
A. waliteseka hadi siku yao ya mwisho
B. hawakumsaidia mtoto wao
C. walimlipia Matatizo karo hadi katika chuo kikuu
D. walifurahia maisha baada ya mtoto wao kupata kazi.

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Wazazi wengi wanaichukulia michezo ya watoto kama shughuli isiyo na maana. Kimsingi, ipo imani inayojengeka kuwa kucheza ni kupoteza muda. Matokeo yake ni kuwa wazazi hujitahidi kuwazuia watoto wasicheze kwa matumaini ya kuwasaidia wapate muda wa kufanya mambo ya maana zaidi kama vile kusoma na kukamilisha kazi za kiada na ziada. Pamoja na umuhimu wa kufanya hivyo, hata hivyo, michezo inabaki kuwa shughuli yenye umuhimu mkubwa katika ukuaji wa jumla wa mtoto kimaarifa, kimahusiano, kimwili na kihisia. Michezo ni shughuli zisizo rasmi anazozifanya mtoto kwa lengo la kufurahi na kuburudika. Michezo hiyo ni kama vile kubembea, kuteleza, kuogelea na kadhalika.

Awali ya yote, kukua kiakili kwa mtoto hutegemea kwa kiasi kikubwa namna anavyoweza kucheza. Kwa kawaida, mtoto hujulikana iwapo yu timamu baada ya kuzaliwa kwa kuangalia kiwango chake cha kushughulisha viungo vya mwili wake. Kupitia michezo, mtoto hutumia akili kujifunza namna ya kutatua changamoto zinazomkabili. Mathalani, anapojifunza kuruka kamba, inabidi aelewe namna ya kutua kwa miguu yake inavyotakiwa kupishana na kamba inayopita chini. Zoezi kama hili, mbali na kumsaidia kuchangamsha viungo vyake, pia linamkuza kiufahamu.

Kucheza pia kunamhitaji mtoto atumie viungo vya mwili. Ili acheze '**rede**', kwa mfano, ni lazima aruke, akimbie kukwepa au kuufuata mpira, lazima atumie mikono yake kujaza mchanga kwenye chupa na vitendo vingine vinavyofanyika kwa haraka, ambavyo kwa kweli ni kufanya mazoezi ya mwili. Tafiti nyingi zimeonesha namna kutocheza kunakokwenda sambamba na utazamaji wa televisheni kunavyoweza, kwa kiasi kikubwa, kuchangia kuongeza tatizo la uzito mkubwa wa mwili kwa watoto. Kucheza ni hatua ya kukabiliana na tatizo hili na kunasaidia kupunguza uwezekano wa magonjwa yanayosababishwa na kukosa mazoezi. Ili iwe na msaada, hata hivyo michezo hiyo ni muhimu ihusishe kwa kiasi kikubwa viungo vya mwili.

Michezo ni mawasiliano. Ili waweze kucheza vizuri, watoto hulazimika kujadiliana mambo ya msingi kama aina ya mchezo utakaochezwa, jukumu la kila mmoja, kanuni zitakazoongoza mchezo na kadhalika. Aidha, ni kawaida watoto kupenda kuimba, kueleweshana, kuhojiana na hata kujieleza pale kanuni zilizowekwa zinapovunjwa na mmoja wao. Haya yote huwasaidia kujifunza wenzao wanavyoongea, wanavyotumia maneno, wanavyojieleza pale wanapokosea na hivyo kukuza uwezo wao wa kuelewa kanuni za lugha.

**Kucheza hujenga uwezo wa watoto kushirikiana**, kufanya kazi pamoja, kufanya maamuzi yanayokubalika na pande zote, kutatua migogoro na wakati mwingine kujifunza kukosa kile wanachokitamani. Haya ni maeneo muhimu yanayokuza uwezo wa kujenga maelewano. Kwa kawaida, si kila kanuni inayoongoza mchezo hukubaliwa na watoto wote. Mazingira hayo huhitaji uwezo wa kushawishi wengine lakini pia huwa ni fursa ya kumfundisha mtoto kujifunza kuyaona mambo kwa macho ya wengine.

41. Aya ya kwanza inaeleza kuwa:
   A. michezo ya watoto ni shughuli isiyo na maana
   B. wazazi wengi wanaichukulia michezo ya watoto kuwa shughuli ya maana
   C. wazazi wote wanaichukulia michezo ya watoto kuwa shughuli isiyo na maana
   D. wazazi wengi wanaichukulia michezo ya watoto kuwa shughuli isiyo na maana.

42. Kulingana na aya ya kwanza, ni nini ambacho wazazi wanachukulia kuwa muhimu zaidi?
   A. Kucheza na watoto wao.
   B. Kufanya kazi za shuleni.
   C. Kula vizuri
   D. Kuwasaidia kufanya kazi za nyumbani

43. Mwandishi anaeleza kuwa michezo hufanywa na watoto kwa lengo gani?
   A. Kufurahi na kuburudika.
   B. Kuchangamka na kusoma.
   C. Kuelimika na kuchoka.
   D. Kufurahi na kushindwa.

44. Gani **si** faida ya michezo kulingana na ufahamu?
   A. Husaidia ukuaji wa akili.
   B. Huimarisha viungo vya mwili.
   C. Husaidia katika mawasiliano.
   D. Huhitaji matumizi ya pesa nyingi.

45. **Aya ya tatu** inafafanua kwamba;
   A. utazamaji runinga hupunguza uzito wa mwili
   B. michezo inayohusisha viungo vya mwili si muhimu
   C. michezo huweza kuimarisha afya
   D. michezo huongeza uwezekano wa kupata magonjwa.

46. **'Kucheza hujenga uwezo wa watoto kushirikiana'** Ni methali gani inayoafikiana na kauli hii?
   A. Baada ya dhiki ni faraja.
   B. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.
   C. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.
   D. Mchezea tope humrukia.

47. Aya ya mwisho inaeleza kuwa michezo huwasaidia watoto kufanya nini?
   A. Kujifunza kutamani walichokikosa.
   B. Kuharibu uwezo wa kujenga maelewano.
   C. Kuyaona mambo kwa macho yao.
   D. Kujifunza kukosa kile wanachokitamani.

48. Aya ya nne inaeleza kuwa michezo;
   A. husaidia mawasiliano ya mtoto
   B. hujenga mwili wa mtoto
   C. husaidia akili ya mtoto
   D. hujenga uchumi wa mtoto.

49. Yawezekana kuwa mtoto ambaye hachezi;
   A. atakuwa na afya bora
   B. atakumbwa na matatizo mbalimbali
   C. atafanya vizuri sana masomoni
   D. atakuwa na marafiki wengine sana.

50. Kwa mujibu wa kufungu, **si** kweli kuwa
   A. wazazi wanafaa kuwaruhusu watoto wacheze
   B. michezo huweza kuleta amani kati ya watoto
   C. michezo ina faida nyingi
   D. watoto wanafaa kucheza wakati wote.